

# HALMASHAURI YA MANISPAA KIGAMBONI



25/08/2022

## TANGAZO LA ZABUNI

### MARUDIO

#### **ZABUNI YA USAFI, UZOAJI NA USAFIRISHAJI WA TAKA NGUMU KATIKA MITAA YA MANISPAA YA KIGAMBONI ZABUNI NAMBA LGA/181/NCS/2022/2023/02**

1. Halmashuri ya Manispaa ya Kigamboni inakaribisha maombi ya wananchi walio na nia ya kufanya kazi ya Usafi, uzoaji na usafirishaji wa taka ngumu kwa njia ya Ubinafsishaji katika mitaa mbalimbali ndani ya Manispaa ya Kigamboni
2. Kwa wenye nia ya kufanya kazi wanaweza kuwa ni watu binafsi, Taasisi, Kampuni au vikundi (ushirika) vilivyoanzishwa kwa kazi ya kukusanya taka ngumu.
3. Maombi yawe katika nakala halisi (**Original**) na nakala mbili za kudurufu zinazofana zilizojazwa kwa usahihi zikitaja mtaa na Kata ambazo muombaji atafanya kazi. Bahasha hizo zifungwe vizuri katika bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa zabuni namba **LGA/181/NCS/2022/2023/02** ya **Usafi, uzoaji na usafirishaji wa taka ngumu katika Manispaa ya Kigamboni.**

4. Mitaa inayohusika katika Tangazo hili ni kama ilivyoorodheshwa kwenye jedwali hapa chini:-


<b>Na.</b>	<b>Jina la Kata</b>	<b>Mtaa</b>
1	KIGAMBONI	Ferry
2	TUNGI	Magogoni
3	SOMANGILA	Malimbika
		Dege
		Visikini
4	KISARAWA II	Kichangani Tumaini Mwasonga Mwaninga Vumilia ukooni

5. Maombi yaliyofungwa kwa LAKIRI (**Seal**) yatumwe kwa;-

**Katibu wa Bodi ya Zabuni,  
Halmashuri ya Manispaa ya Kigamboni,  
S.L.P 36009 Dar es Salaam”.**

6. Muombaji anapomba anapaswa kutamka, kuzingatia na kuambatanisha vitu vifuatavyo:-
- Muombaji kama ni Taasisi au Kampuni aambatanishe nyaraka zote za usajili wa Taasisi au Kampuni hiyo.
  - Muombaji aambatanishe nakala ya mikataba ya kazi zinazofanana na hizo alizowahi kufanya.
  - Muombaji anapaswa kufanya utafiti wa kutosha kabla ya kuomba zabuni ikiwa ni pamoja na kutembelea eneo la kazi (**site visit**) ili aweze kufahamu ukubwa wa mtaa/Kata.
  - Muombaji asiwe anadaiwa **AU** kuwa na Mgogoro na Halmashuri ya Manispaa ya Kigamboni.
  - Kwa kutokuelewa Kipengele chochote unaombwa kufika **Ofisi ya Katibu wa Bodi ya zabuni, Halmashuri ya Maispaa ya Kigamboni** iliyopo Halmashuri ya Manispaa ya Kigamboni eneo la Gezaulole kwa ajili ya kupatiwa Ufafanuzi Zaidi.

- f. Mwisho wa Kupokea maombi haya ni tarehe **31/08/2022**, **Saa 5.00** Asubuhi na ufunguzi utafanyika hadharani katika Ofisi ya Katibu wa Bodi ya zabuni, Halmashuri ya Manispaa ya Kigamboni **5.30 asubuhi siku hiyo hiyo** mbele ya wawakilishi wa waombaji watakaopenda kuhudhuria katika ufunguzi huo utakaofanyika katika Ukumbi mdogo wa mikutano Manispaa ya Kigamboni.
- g. Zabuni zitakazochelewa hazitapokelewa.

  
**Erasto N. Kiwale**  
**MKURUGENZI WA MANISPAA**  
**KIGAMBONI**

MKURUGENZI WA MANISPAA  
KIGAMBONI